VERMONT
DEPARTMENT OF HEALTH

# Kufunga Ndoa huko Vermont

## Maswali na Majibu ya Kukusaidia Kupanga Harusi Yako huko Vermont

1. **Je, nani anaweza kufunga ndoa huko Vermont?**

   Watu wawili ambao kila mmoja ana umri wa angalau miaka 18 wanaweza kufunga ndoa ya kiserikali huko Vermont.

2. **Je, kuna vikwazo vingine vyovyote vya ndoa?**

   Mtu yeyote aliye chini ya ulezi hawezi kufunga ndoa bila idhini ya maandishi ya mlezi. Vermont pia hairuhusu ndoa kati ya jamaa wa karibu zaidi. Huwezi kufunga ndoa na mzazi, babu/bibi, dada, kaka, mtoto, mjukuu, mpwa wa kike, mpwa wa kiume, shangazi au mjomba. Huwezi kufunga ndoa ikiwa mmoja wenu amefunga ndoa na mtu mwingine kwa sasa au ikiwa mmoja wenu ameunganishwa katika muungano wa kiserikali na mtu mwingine. Sheria inawahitaji wahusika wote wawili kuwa na akili timamu.

3. **Je, tunahitaji leseni ya ndoa? Je, tunahitaji kufanya vipimo vya damu?**

   Mtahitaji leseni lakini hamhitaji kufanya vipimo vya damu na hakuna kipindi cha kusubiri.

4. **Je, tutapata wapi leseni ya ndoa na inagharimu pesa ngapi?**

   Mnaweza kupata leseni kutoka kwa karani yeyote wa mji/jiji la Vermont na gharama ni $80. Leseni hiyo ni halali kwa siku 60 kuanzia tarehe inapotolewa. Katika wakati huo, mtu aliyeidhinishwa lazima afanye sherehe yenu ya harusi — vinginevyo, leseni inakuwa batili.

5. **Je, tunapaswa kutoa maelezo yapi ili kupata leseni ya ndoa?**

   Kando na maelezo ya msingi kuwahusu (majina, miji ya makazi, mahali na tarehe za kuzaliwa), lazima pia mseme majina ya wazazi wenu, ikiwemo majina ya kuzaliwa ya mama zenu (majina ya ukoo kabla ya ndoa), na mahali walikozaliwa. Nakala zilizoidhinishwa za vyeti vyenu vya kuzaliwa zinaweza kusema mengi kati ya maelezo haya. Pia mtaombwa kutoa maelezo kuhusu idadi ya ndoa na miungano ya kiserikali ya awali, na jinsi na wakati ilipoisha. Maelezo haya ni ya siri na sio sehemu ya cheti cha ndoa. Sheria ya Vermont inahitaji wahusika wote wawili watie saini kwenye ombi kuthibitisha usahihi wa maelezo mliyotoa. Karani wa mji atakagua ombi hilo ili kuthibitisha kwamba maelezo yaliyotolewa hayaonyeshi kwamba mmepigwa marufuku kufunga ndoa huko Vermont na kwamba nyote wawili mmetia ombi saini. Kisha karani wa mji atatoa leseni ikiwa angalau mmoja wenu ametia leseni saini mbele ya karani.

6. **Je, itakuwaje ikiwa mmoja wetu alikuwa amefunga ndoa au kuwa katika muungano wa kiserikali hapo awali?**

   Ikiwa mume, mke au mwenzi wako wa muungano wa kiserikali amefariki, uko huru kufunga ndoa. Karani atauliza tarehe ambayo mume/mke wako au mwenzi wako wa muungano wa kiserikali alifariki. Ikiwa umetalikiwa, unaweza kufunga ndoa tena baada ya tarehe ambayo ndoa yako ya awali au muungano wako wa kiserikali wa awali ulivunjwa kisheria. Ikiwa nyinyi ni wenzi katika muungano uliopo wa kiserikali, mna uhuru wa kuoana.

7. **Je, leseni inaweza kutolewa kupitia barua? Je, tunaweza kufunga ndoa bila mmoja wetu kuwepo?**

   Hapana. Leseni ya ndoa haiwezi kutolewa kupitia barua na hamuwezi kufunga ndoa bila mmoja wenu kuwepo.

8. **Je, tunaweza kufunga ndoa wapi?**

   Mkiwa na leseni halali ya Vermont, mnaweza kufunga ndoa mahali popote ndani ya Vermont, lakini ndani ya Vermont tu.

**9. Je, nani anaweza kutufungisha ndoa? Je, tunahitaji mashahidi?**

Jaji wa Mahakama ya Juu, jaji wa mahakama kuu, jaji wa wilaya, jaji wa kuthibitisha mirathi, jaji msaidizi, hakimu wa amani au kasisi aliyefanywa kasisi rasmi au mwenye leseni anayeishi Vermont anaweza kufanya sherehe yenu ya harusi. Kasisi anayeishi katika jimbo au nchi inayopakana anaweza kuwafungisha ndoa ikiwa kanisa lake, hekalu, msikiti au shirika lingine la kidini linapatikana ndani ya Vermont au sehemu ya Vermont. Kasisi anayeishi katika jimbo lingine au Kanada anaweza kuwafungisha ndoa ikiwa kwanza atapata idhini maalum kutoka kwa mahakama ya uthibitishaji wa mirathi katika wilaya ambapo ndoa itafungwa. Aidha, mtu yeyote ambaye ana umri wa zaidi ya miaka 18 anaweza kujiandikisha kwa Katibu wa Jimbo ili kuwa mfungisha ndoa wa muda. Mtu ambaye amejaza fomu ya kujiandikisha na ambaye amelipa ada ya kujiandikisha ya $100 atapokea cheti kinachomwidhinisha mtu huyo kufungisha ndoa mahususi ya Vermont. Mamlaka ya mtu huyo ya kufungisha ndoa hiyo yataisha wakati sawa na wa leseni husika. Kwa maelezo kuhusu kujiandikisha kuwa mfungisha ndoa wa muda tembelea https://sos.vermont.gov/ au upige simu kwa 802-828-2363. Sheria ya Vermont haihitaji mashahidi, lakini, ikiwa unapanga sherehe ya kidini, peleleza ili kuona ikiwa kanuni za dini hiyo zinahitaji mashahidi.

**10. Je, tutaifanyia nini leseni hiyo? Je, nini huifanyikia baada ya sherehe?**

Kwa mujibu wa sheria, nyote wawili lazima mtie saini leseni na kuwasilisha leseni hiyo kwa mtu atakayeongoza sherehe yenu ya harusi kabla ya ndoa kufungwa. Baada ya sherehe hiyo, mtu atakayefanya sherehe (mfungisha ndoa) atajaza sehemu kuhusu tarehe, mahali na maelezo kuhusu mfungisha ndoa na kutia leseni yenu saini. Kuanzia hapo, leseni hiyo huwa cheti cha ndoa. Mfungisha ndoa lazima arejeshe cheti hicho kwa ofisi ya karani wa mji ambapo ilichapishwa ndani ya siku 10 baada ya harusi, ili ndoa yenu iweze kusajiliwa rasmi. Ikiwa mfungisha ndoa amejiandikisha kwa Katibu wa Jimbo kama mfungisha ndoa wa muda, nakala ya cheti cha idhini kilichotolewa na Katibu wa Jimbo inapaswa kuambatishwa kwenye cheti kilichotiwa saini na kurejeshwa kwa ofisi ya karani.

**11. Je, tutapataje nakala ya cheti chetu cha ndoa?**

Wakati wa kununua leseni yenu ya ndoa, mnaweza kupanga na karani wa mji awatumie kwa barua nakala iliyoidhinishwa ya cheti chenu mara tu ndoa yenu inaporekodiwa. Gharama ni $10 kwa nakala iliyoidhinishwa pamoja na $80 kwa ununuzi wa leseni ($10 + $80 = $90). Au, wiki mbili au zaidi baada ya sherehe, mnaweza kuomba, ana kwa ana au kwa maandishi, nakala za ziada kutoka kwa ofisi ya karani wa mji ambako mlinunua leseni yenu kwa ada sawa ya $10. Au, wiki sita au zaidi baada ya sherehe yenu, mnaweza kuomba, ana kwa ana au kwa maandishi, nakala iliyoidhinishwa kutoka kwa Idara ya Afya ya Vermont, Ofisi ya Rekodi Muhimu kwa $10. Kwa njia yoyote ile, mtapokea nakala ya cheti asili, iliyochorwa muhuri wa mji au jimbo, kutiwa saini na kuandikwa tarehe na afisa anayefaa.

*Ilisasishwa tarehe 1 Julai, 2023*